

# Wakaguzi wa ndani washauriwa kuangalia tija miradi ya Tehama

Na Mwandishi Wetu

**M**KAGUZI Mkuu wa Ndani Msaidizi Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, Paison Mwamnyasi, amewataka wakaguzi wa ndani kutoa ushauri wenyewe tija kwa serikali katika miradi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kwa kuzingatia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao.

Mwamnyasi alisema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa awamu ya pili ya mafunzo maalumu kwa wakaguzi wa ndani kutoka halmashauri na tawala za mikoa 13 za Tanzania Bara.

Alisema mafunzo ya ukaguzi wa mifumo na miradi ya Tehama serikalini ni muhimu kwa wakaguzi wa ndani kwa kuwa yanawajengea uwezo katika utendaji kazi na kurahisisha shughuli za ukaguzi na kutoa ushauri wenyewe tija kwa serikali.

"Ukielewa namna mifumo inavyofanya kazi, unaweza kukagua ipasavyo, na tutaeuka kutaja majina ya watu katika taarifa zetu za ukaguzi badala ya mifumo," aliongeza.

Aidha, Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa Tehama Mamlaka ya Serikali Mtandao, Sylvani Shayo aliwasilitiza wakaguzi wa ndani kutumia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao wakati wa kusimamia na kufanya ukaguzi.

Meneja wa Udhibiti wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, Sultana Seiff alisema serikali mtandao haitaki kuacha kada yoyote nyuma katika matumizi ya Tehama kwa kuwa dunia ya sasa inaendeshwa kidijiti, hivyo wakaguzi wa ndani wanapewa mafunzo hayo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mafunzo hayo ya siku tano yanayofanyika mkoani Morogoro yanahuisha wakaguzi wa ndani 110 kutoka halmashauri na Tawala za mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida, Kigoma, Mara, Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Rukwa, Kagera, Geita, Simiyu na Katavi.